

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S. L.P 1575,
Simu: (026) 2700157
Nukushi: (026) 2703014
Barua pepe: rbciringa@pccb.go.tz
Mtandao : www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

IRINGA 10 JULAI, 2020

**TAKUKURU IRINGA YAMKABIDHI MWALIMU SHILINGI 19,460,000/-
ALIZODHULUMIWA NA MKOPO BAMIZA.**

Ndugu wanahabari,

Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Iringa katika operesheni inayoendelea ya kuwadhhibiti wanaojihusisha na mikopo umiza, imefanikiwa kurejesha fedha kiasi cha Shilingi **19,460,000/=** kwa Mwalimu Mstaafu **Bw. Msuri Selemani Chuma** kutoka kwa *Magere Credit Company Limited* na *Dicta Financial Services Company Limited*.

Mnamo mwezi Disemba, 2019 **Bw. Msuri Selemani Chuma** alikopa fedha shilingi **11,900,000/=** kutoka kwa *Magere Credit Company Limited* inayomilikiwa na **Bw. Juma George Magere** kwa ajili ya kwenda kulipia ada za watoto wake wapatao 5 pamoja na yatima 2 wanaosoma Sekondari na Vyuoni.

Ndugu wanahabari,

Mara baada ya kukopa fedha hizo alitakiwa kurejesha marejesho ya jumla ya shilingi **31,425,000/=** yakiwa na riba ya asilimia 264, ambapo kati ya hizo alikuwa amefanikiwa kurejesha shilingi **1,065,000/=** na hivyo kusalia rejesho la shilingi **30,360,000/=**. Aidha, dhamana ya mkopo huo ilikuwa ni vyeti vya elimu yake, kadi mbili za benki pamoja na nywila (password).

Baada ya taarifa hii kupokelewa na kufanyiwa kazi, yalibainika mapungufu ya utozaji wa riba kinyume na taratibu za utozaji wa riba za mikopo jambo ambalo wahusika wa mikopo hiyo walikiri mapungufu hayo.

Ndugu wanahabari,

Kutokana na mapungufu hayo walimtoza mkopaji riba stahiki ambapo katika mkopo wa shilingi **11,900,000/=** alirejesha shilingi **14,000,000/=** badala ya shilingi **30,360,000/=**. Na katika mkopo wa shilingi **1,000,000/=** alirejesha shilingi **1,400,000/=** badala ya shilingi **4,500,000/=**.

Hivyo, Bw. Msuri Selemani Chuma alitakiwa kufanya marejesho ya jumla shilingi **34,860,000/=** lakini baada ya TAKUKURU kufanyia kazi suala hili, alirejesha jumla ya shilingi **15,400,000/=** na hivyo kuokoa fedha kiasi cha shilingi **19,460,000/=** ambazo bila TAKUKURU kuingilia kati angedhulumiwa (kupigwa).

Ndugu wanahabari,

TAKUKURU inatoa wito kwa wananchi wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na ukiukaji wa Sheria na taratibu za mikopo kuacha vitendo hivyo mara moja. Aidha Wananchi wanapobaini vitendo hivi wanatakiwa kutoa taarifa ili hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Imetolewa na:

SGN

Mweli E. Kilimali

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Iringa